# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI KWA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KUPITIA RIPOTI YA KAMATI YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia Uhai na Afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza vyema majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi. Vile vile, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako kwa mnavyosimamia chombo hiki muhimu na kwa uadilifu wa hali ya juu ili kufikia malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na Mipango na Mikakati mbali mbali ya Kitaifa katika kukuza demokrasia.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia, kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake uliotukuka ambapo ndani ya muda mfupi tu wa miaka miwili tumeona mambo aliyowafanyia wananchi wetu na kila mmoja ni shahidi katika mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii. Kamati inaridhika sana na juhudi za Mheshimiwa Rais za kutembelea maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kutatua matatizo ya wananchi. Kamati

inamuomba Mwenyezi Mungu kumzidishia afya njema, hekma na busara katika kuwatumikia wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Harous Said Suleiman kwa uweledi wake uliomfanya aweze kuteuliwa kuwa Waziri katika Ofisi hii pamoja na kuwapongeza watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Omar Dadi Shajak kwa mashirikiano yao wanayotupatia wakati wa shughuli zetu za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao mkubwa uliowawezesha kujadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali ambayo yametolewa ufafanuzi na Ofisi hii kwa lengo la kuhakikisha kwamba utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa ndani ya ripoti ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2021/2022 chini ya Taasisi zake; majibu yake yamekuwa ni sahihi na yanauhalisia katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima naomba sasa uniruhusu kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kutumia Kanuni ya 107(3) inapewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia. Ambapo kazi hii ilifanywa vyema kwa kipindi hiki kilichopita na bado Kamati inazidi kufuatilia utekelezaji wa maoni hayo kila inapoona inafaa kufanya.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya *109(15)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, imetoa fursa ya lazima kwa kila Kamati kutayarisha ripoti ya mwaka itakayowasilishwa katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kanuni ya *108(17)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa maoni na ushauri huo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika kujadili utekelezaji huo unaojumuisha maoni na ushauri wa Kamati kwa wizara na taasisi zake inazozifanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inaelekeza kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, jumla ya maoni kumi na saba (*17)* yaliyoagizwa na Kamati katika mwaka wa fedha *2021/2022.*

## Utekelezaji wa Maagizo

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati yetu imeridhishwa sana na utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kupitia ripoti yetu ya mwaka jana, isipokuwa kutokana na changamoto mbali mbali zinzoikabili Wizara hii kupitia Taasisi zake mbali mbali, tunaiomba Serikali kuzidisha juhudi zake katika kuzisaidia Taasisi Programu zao kutekelezwa kwa kuziondoa changamoto kadhaa zinazoikabili Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza juhudi za kupambana na janga la dawa za kulevya hapa nchini, Kamati imeelezwa kwamba Serikali kupitia Ofisi hii imesaini hati ya makubaliano na "British High Commission" ili Shirika hili liweze kuipatia

Zanzibar kifaa maalum na cha kisasa ambacho kitatumika kuongeza kasi ya upekuzi kwa upande wa madawa ya kulevya katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati inashauri utakapo kamilika mpango huu kwa upande wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar basi huduma hii pia ipelekwe na Uwanja wa Ndege Pemba pamoja na kuongeza nguvu katika bandari zote za Unguja na Pemba. Sambamba na hayo, Kamati inaipongeza Mamlaka kwa kutoa namba maalum ambayo itawasaidia wananchi kutoa taarifa za uhalifu wa Dawa za Kulevya katika jamii kwa usiri na bila kuwepo kwa usumbufu wowote kwa watoa taarifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa "Waswahili husema mcheza kwao hutunzwa" basi na Mamlaka imeandaa tunzo maalum kwa ajili ya watu wote wenye nia njema ya kuisaidia Serikali dhidi za mapambano ya Dawa za Kulevya. Kwa hivyo, bajeti maalum imetengwa kwa ajili ya kuwapatia zawadi wale wote wenye kutoa taarifa ya uhalifu wa Dawa za Kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tume ya UKIMWI Zanzibar Kamati imeridhishwa na majibu yaliyotolewa mbele ya Kamati kwa namna ambavyo Tume hii imekuwa ikitekeleza majukumu yake. Aidha, ni vyema Serikali kuzidisha nguvu katika kuzisaidia Jumuiya zote ambazo zinapambana na UKIMWI pamoja na magonjwa ya uasharati ili kuzifikia jamii na kukuza elimu ya kinga na kujitambua.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mamlaka na Idara ya Mazingira Zanzibar Kamati inaipongeza Mamlaka kwa kutekeleza vyema maoni na ushauri wa Kamati na tunaishauri Mamlaka hii kuzidisha kasi katika udhibiti na uhifadhi wa

mazingira. Aidha, Kamati imeitaka Mamlaka kuharakisha zoezi la marekebisho ya Sheria yake ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** tunafahamu kwamba Serikali yetu imekuja na nia njema kabisa ya kuanza kuvikodisha visiwa vidogo vidogo kwa wawekezaji kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi na maendeleo kwa watumiaji wa visiwa husika. Kamati imeridhishwa na sera hii na inaishauri jamii kuunga mkono juhudi hizi za Serikali yetu. Aidha, Kamati inashauri wawekezaji ambao watakodishwa visiwa hivi basi ni vyema kupewa na masharti ni mikakati iliyopo katika kuvitunza na kulinda mazingira ya visiwa hivi kw ajili ya matumizi ya sasa na vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine Kamati inashauri Serikali kubainisha Taasisi halisi yenye dhamana kisheria katika kusimamia uhifadhi wa visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar ambapo Taasisi hiyo itafahamika na jamii yote kuwa ndio yenye dhamana ya usimamizi wa visiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia, Kamati inapenda kuchukuwa fursa hii kuishauri jamii kutoa mashirikiano na Mamlaka ya Mazingira kwa kudumisha usafi na uhifadhi wa mazingira kwa kupinga matumizi ya mifuko ya plastiki na kutoa taarifa kwa wafanyabiashara wenye kuingiza mifuko ya plastiki na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni machache sana kwa niaba ya Kamati yangu pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kuwa watulivu na kunisikiliza muda wote wa kuwasilisha maoni haya.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ***Naomba Kuwasilisha.***

Ahsante,

……………………………..

(Mhe. Machano Othman Said)

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**